

Imetolewa tarehe 10 Februari, 2009

MIKUTANO KATI YA TFDA NA WASINDIKAJI NA WAINGIZAJI WA VYAKULA

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) imeandaa mkutano wa siku mbili kati yake na wasindikaji na waingizaji wa vyakula kutoka Mkoa wa Dar es Salaam kujadili pamoja na mambo mengine mikakati ya kuleta ufanisi katika shughuli za udhibiti wa vyakula sambamba na ukuzaji wa sekta ya viwanda nchini.

TFDA inakabiliana na changamoto mbalimbali katika usimamizi wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi namba 1 ya mwaka 2003 ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria kwa hiari miongoni mwa wasindikaji na waingizaji wa vyakula hivyo kuweza kuleta mashaka juu ya usalama wa vyakula vinavyotumiwa.

Mkutano wa kwanza kati ya TFDA na waingizaji wa vyakula umepangwa kufanyika tarehe 11 Februari, 2009 wakati ule wa wasindikaji wa vyakula umepangwa kufanyika tarehe 12 Februari, 2009. Jumla ya waingizaji 80 na wasindikaji wa vyakula 73 wamealikwa kwenye mikutano hiyo.

Mikutano hiyo miwili itafanyika kwenye ukumbi wa mikutano ulioko TFDA Makao Makuu. Mkutano wa kwanza utafunguliwa na Mganga Mkuu Kiongozi (Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii) Dkt. Deo Mutasiwa wakati ule wa pili utafunguliwa na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Dkt. D. Mbando aliye chini ya Wizara hiyo hiyo.

Mada mbalimbali zitawasilishwa zikilenga katika:

- Kuwawezesha waingizaji wa vyakula kufahamu mahitaji ya Kisheria juu ya uingizaji wa vyakula nchini kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi namba 1 ya mwaka 2003 na Kanuni zilizotengenezwa chini yake.
- Kueleweshwa wasindikaji wa vyakula juu ya mahitaji ya Kisheria ya shughuli za usindikaji wa vyakula nchini.
- Kuhimiza utekelezaji wa hiari wa matakwa ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2003 kwa wasindikaji na waingizaji wa vyakula.
- Kujadiliana juu ya mikakati ya kuongeza ufanisi katika uzingatiaji wa Sheria na kuongeza uwezo wa vyakula vinavyozalishwa ili kumudu ushindani wa soko la ndani na nje kutokana na ubora na usalama wake pia kukuza sekta ya viwanda vya kusindika vyakula nchini.

Inatarajiwa kuwa katika mikutano hiyo TFDA, wasindikaji na waingizaji wa vyakula watajadiliana na kufikia makubaliano juu ya kuongeza ufanisi katika shughuli za udhibiti wa vyakula Tanzania kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii inalindwa dhidi ya madhara ya kiafya yanayoweza kusababishwa na ulaji wa vyakula visivyofaa.